



Knowledge grows

Fuga Kibiashara na Lishe Bora Toka Yara



1. Fomula Wakati Masika

Masika huwa na mvua nyingi na majani ya kijani, lakini majani ya kijani yana upungufu wa madini ya Phosphate kwa kiwango kikubwa ambayo inapelekea umuhimu wa kutumia fomula hii kwa mifugo yako.

Fomula

Kimtrafos 12 grande	Chumvi	Jumla
50kg	50kg	100kg

Faida kwa Mifugo Yako

- ✓ Huzuia tabia kula takataka kama udongo, plastiki au vitu vingine visivyofaa.
- ✓ Husaidia mifugo kupenda kunywa maji
- ✓ Huongeza hamu ya kula na kusaidia mmeng'enywa wa chakula
- ✓ Husaidia ukuaji wa haraka na kuongeza uzalishaji wa maziwa.



Kiwango cha Ulishaji

Ng'ombe	Mbuzi/Kondoo	Wanyama Pori
100 – 240 gramu kwa siku	18 – 36 gramu kwa siku	0.6 gramu kwa siku

2. Wakati wa Kiangazi

Kiangazi ni kipindi cha ukame, ambapo majani huwa makavu na yenye upungufu wa madini na protin. Hii hupelekea umuhimu wa kutumia fomula hii kwa mifugo yako.

Fomula

Pumba	250 kg
Mashudu	150 kg
Chumvi	350 kg
Feed Grade Urea	100 kg
Kimtrafos 12 Grande	100 kg
Kalori 3000	50 kg
Feed Grade Sulphur	5 kg
Jumla	1005 kg



Faida kwa Mifugo Yako

- ✓ Hunenepesha mifugo hata wakati wa nyasi kavu.
- ✓ Husaidia kuongeza uzalishaji wa maziwa na ubora wa nyama ili kukuza kipato chako.
- ✓ Huimarisha afya ya kizazi na kuongeza uzaaji wa mifugo yako.
- ✓ Husaidia mmeng'nyo wa nyasi kavu ndani ya tumbo la mifugo.

Kiwango cha Ulishaji

Ng'ombe	Mbuzi
450- 650 gramu kwa siku	80 – 120 gramu kwa siku

TAHADHARI:

Usiwape mifugo wenye njaa fomula yenye Feed Grade Urea.
Wape baada ya kula malisho.

3. Flushing

Fomula

Pumba	550 kg
Mashudu	150 kg
Chumvi	250 kg
Feed Grade Urea	75 kg
Kimtrafos 12 Grande	75 kg
Kalori 3000	50 kg
Feed Grade Sulphur	5 kg
Jumla	1155 kg



Faida za Formula ya Flushing kwa Kondoo (Sheep)

- ✓ Huongeza uwezekano wa kondoo kuzaa mapacha au zaidi.
- ✓ Huongeza uwezekano mkubwa wa kondoo jike kushika mimba kirahisi

Faida za Fomula ya Flushing kwa Ng'ombe (Cows)

- ✓ Kusaida kushika mimba ndani ya miezi 3 baada ya kuzaa.
- ✓ Husaidia ongezeko la ndama kila mwaka

Kiwango cha Ulishaji

Kondoo	Ng'ombe
100- 200 gramu kwa siku	800 – 1200 gramu kwa siku



4. Starter

Fomula

Mahindi ya njano yaliyo balazwa	66 kg
Unga wa Mashudu (Allzeti au Pamba)	16 kg
Unga wa Dagaa	6 kg
Unga wa Lusina	11 kg
Kimtrafos 12 Grande	1 kg
Jumla	100 kg



Faida kwa mifugo yako

- ✓ Huchochea wa ukuaji wa haraka wa ndama
- ✓ Inaimarisha tumbo la ndama kuzoea kuanza kula majani na chakula
- ✓ Ni mbadala wa maziwa kwa ndama.
- ✓ Inapunguza msongo wa mawazo anapoachishwa maziwa
- ✓ Huimarisha afya na kinga kwa ndama

Kiwango cha Ulishaji

Ndama ua Mtoto wa kondoo

Kiwango chochote atachoweza kula

5. Mchanganyiko wa Kuongeza Ubora wa Malisho

Fomula

Feed Grade Urea	15 kg
Feed Grade Sulphur	0.75 kg
Kalori 3000	25 kg
Maji	200 lita



Faida kwa Mifugo Yako

- ✓ Huongeza hamu ya kula kwa majani yasiyolika
- ✓ Rafiki Mzuri wa mazingira, badala ya mabua ya mazao kutupwa basi hutumika kama chakula kwa mifugo.
- ✓ Husaidia kuongeza uzito kwa mifugo
- ✓ Kurahisisha mmeng'enywa wa malisho makavu kwenye tumbo la mifugo

Jinsi ya Kuchanganya na Kutumia

Nyunyiza mchanganyiko juu ya malisho: lita 2 kwa kilo 10 za malisho. Usitengeze malisho mengi kwa wakati mmoja ili kuzuia ukungu/fangasi na kupotea kwa Urea, ambayo ni muhimu kwa uzalishaji wa protini mwillini mwa mifugo. Tengeza malisho ya kutosha kwa siku 4-5 tu.

ZINGATIA: Usilishe mifugo yako malisho yalichanganywa na Feed Grade Urea na fomula zenye Feed Grade Urea kwa siku moja.

Lishe Bora za Mifugo Toka Yara

6. Fomula ya Ng'ombe Mwenye Mimba

Ni fomula inayosaidia ng'ombe anapokaribia kuzaa asipate changamoto ya milk fever (homa ya maziwa)

Fomula

Kynofos 21	Chumvi	Pumba	Magnesium sulphate
100kg	50kg	50kg	10kg

Faida kwa mifugo yako

- ✓ Huzuia homa ya maziwa
- ✓ Husaidia ng'ombe kuzaa kwa urahisi
- ✓ Huimarisha afya ya ng'ombe baada ya kuzaa
- ✓ Huongeza uzalishaji wa maziwa.

Kiwango cha Ulishaji

Lisha ng'ombe wako gramu 250 kwa siku wiki 1 hadi 2 anapokaribia kuzaa.



7. Fomula ya Kunenepesha Mifugo

Faida kwa mifugo yako.

- ✓ Husaidia kunenepesha mifugo yako
- ✓ Kuongeza ubora wa nyama
- ✓ Huimarisha afya na huongeza nguvu kwa mifugo.
- ✓ Inaongeza faida kwa mfugaji – ukuaji wa haraka na uzito zaidi

Kwanza, tengeneza mchanganyiko wenye protini nyingi (High Protein Concentrate - HPC)

Mashudu (pamba au alizeti)	50 kg
Feed Grade Urea	35 kg
Kimtrafos 12 Gr&e	15 kg
Feed Grade Sulphur	2.5 kg
Chokaa	30 kg
Chumvi	7.5 kg
Jumla (HPC 85)	140 kg



Fomula kwa Ajili ya Ng'ombe

HPC 85	Pumba	Mabua ya mahindi	Kalori 3000	Jumla
50kg	700kg	200kg	50kg	1000 kg

Kiwango cha Ulishaji

Ndama wanapaswa kula chakula kiasi cha asilimia 2 hadi 2.5 ya uzito wa mwili wao kila siku. Wanapokuwa wakubwa zaidi, ongeza hadi asilimia 3.5 ya chakula.

Kwa mfano, kama ndama wako ana kilo 150. Inakuwa $150 \times 0.025 = 3.75$, kwa hiyo kila siku unahitaji kumlisha ndama kilo 3.75 za chakula.

Fomula kwa Ajili ya Kondoo au Mbuzi

HPC 85	50 kg
Pumba za mahindi	800 kg
Lusine	100 kg
Kalori 3000	50 kg
Ammonium Sulphate	8 kg
Jumla	1008 kg



Kiwango cha Ulishaji

Kondoo au mbuzi wanapaswa kula chakula kiasi cha asilimia 3 ya uzito wao kila siku. Kwa mfano, kama ana kilo 50. Unatakiwa kupiga hesabu ya $50 \times 0.03 = 1.5$, kwa hiyo unahitaji kilo 1.5 za chakula kila siku.



Wasiliana Nasi:

 Tupigie 0800 750 188 (BURE)
Telephone: +255 746 909093

 Tovuti: www.yara.co.tz



Facebook & Youtube: Yara Tanzania



X (Twitter): TanzaniaYara



Instagram: YaraTanzania